



TANZANIA INSURANCE REGULATORY AUTHORITY

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

**GUIDELINES ON CORPORATE GOOD GOVERNANCE
REQUIREMENTS FOR TANZANIA INSURERS**

**MIONGOZO YA MAHITAJI YA UTAWALA BORA KWA
KAMPUNI ZA BIMA TANZANIA**

Version No. 2.0

Toleo Na. 2.0

DECEMBER 2025

DESEMBA 2025

TABLE OF CONTENTS	YALIYOMO
SECTION ONE: INTRODUCTION	SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI
1.1 Authorization and Powers5	1.1 Uidhinishaji na Mamlaka5
1.2 Citation5	1.2 Nukuuu5
1.3 Background and Rationale5	1.3 Usuli na Mantiki5
1.4 Application7	1.4 Matumizi7
1.5 Objectives7	1.5 Malengo7
1.6 Interpretations7	1.6 Tafsiri7
SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE	SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA
2.1 Board Oversight	2.1 Usimamizi wa Bodi
2.2 Board Requirements	2.2 Mahitaji ya Bodi
2.3 Responsibilities of the Board	2.3 Majukumu ya Bodi
2.4 Independent Directors	2.4 Wakurugenzi Huru
2.5 Board Determination of Independence	2.5 Maamuzi Bodi kuhusu Uhuru
2.6 Structure of the Board	2.6 Muundo wa Bodi
2.7 Chairperson of the Board	2.7 Mwenyekiti wa Bodi
2.8 Establishment of Board Committees	2.8 Uundwaji wa Kamati za Bodi
2.9 Board Audit Committee	2.9 Kamati ya Bodi ya ukaguzi
2.10 Board Investment Committee	2.10 Kamati ya Bodi ya Uwekezaji
2.11 Other Board Committee	2.11 Kamati nyingine za Bodi
2.12 Senior Management and Chief Executive Officer or Principal Officer	2.12 Viongozi Waandamizi na Afisa Mkuu

TABLE OF CONTENTS	YALIYOMO
SECTION THREE: CAPACITY BUILDING FOR BOARD, MANAGEMENT AND STAFF	SEHEMU YA TATU: KUJENGA UWEZO KWA BODI, VIONGOZI WAANDAMIZI NA WAFANYAKAZI
3.1 Capacity Building for Board, Management and Staff	3.1 Elimu endelevu kwa Bodi, Viongozi Waandamizi na Wafanyakazi
SECTION FOUR: SUCCESSION PLANNING	SEHEMU YA NNE: MPANGO WA URITHISHANAJI MADARAKA
4.1 Succession Planning Process	4.1 Mchakato wa Urithishanaji Madaraka
4.2 Succession Planning for Board	4.2 Bodi ya Wakurugenzi
4.3 Senior Management	4.3 Wasimamizi Waandamizi
4.4 Principal officer	4.4 Afisa Mkuu
SECTION FIVE: PERFORMANCE EVALUATION	SEHEMU YA TANO: TATHMINI YA UTENDAJI
5.1 Board Evaluation	5.1 Tathmini ya Bodi
5.2 Evaluation of Board Committees	5.2 Tathmini ya Kamati za Bodi
5.3 Evaluation of Chief Executive Officer or Principal Officer	5.3 Tathmini ya Afisa Mtendaji Mkuu au Afisa Mkuu
SECTION SIX: INTERNAL GOVERNANCE MECHANISMS	SEHEMU YA SITA: MIKAKATI YA NDANI YA UTAWALA
6.1 The Risk Management Framework	6.1 Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi
6.2 Elements of the internal control System	6.2 Vipengele vya Mfumo Udhhibiti wa Ndani
6.3 Changes to the Risk Management Framework	6.3 Mabadiliko katika Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi
SECTION SEVEN: OUTSOURCING ARRANGEMENTS	SEHEMU YA SABA: MIPANGO YA KUTUMIA HUDUMA ZA NJE
7.1 Outsourcing Requirements	7.1 Mahitaji ya Kutumia Huduma za Nje
7.2 Outsourcing Policy	7.2 Sera ya kutumia huduma za nje
7.3 Scope of Areas for Outsourcing	7.3 Mipaka ya Maeneo ya Kutumia Huduma za Nje
7.4 Outsourcing Processes	7.4 Mchakato wa Kutoa Huduma za Nje
7.5 Outsourcing Agreement	7.5 Mkataba wa Kutumia Huduma za Nje

TABLE OF CONTENTS	YALIYOMO
SECTION EIGHT: SUITABILITY OF KEY PERSONS	SEHEMU YA NANE: SIFA ZA WATU MUHIMU
8.1 Chief Executive Officer or Principal Officer	8.1 Mtendaji Mkuu au Afisa Mkuu
8.2 Chief Finance Officer	8.2 Afisa Mkuu wa Fedha
8.3 Head of Underwriting	8.3 Mkuu wa Uandikishaji Bima
8.4 Head of Claims	8.4 Mkuu wa Usimamizi wa Madai
8.5 External Auditor	8.5 Mkaguzi wa Nje
8.6 Actuary	8.6 Mtathimini bima
SECTION NINE: PROHIBITED PRACTICES	SEHEMU YA TISA: MAMBO YALIYOKATAZWA
8.1 Prohibited Practices	8.1 Mambo yaliyokatatzwa
SECTION TEN: SUPERVISION AND MONITORING	SEHEMU YA KUMI: USIMAMIZI NA UFUATILIAJI
9.1 Enforcement	9.1 Utekelezaji
9.2 Notification on Key Changes	9.2 Taarifa Kuhusu Mabadiliko Muhimu
9.3 Reporting Requirements	9.3 Utoaji wa Taarifa
9.4 Record Keeping	9.4 Uwekaji wa Kumbukumbu
SECTION ELEVEN: REVIEW AND APPROVAL	SEHEMU YA KUMI NA MOJA: MAPITIO NA UIDHINISHAJI
10.1 Review of the Guidelines	10.1 Mapitio
10.2 Effective date	10.2 Tarehe Rasmi ya kutumika
10.3 Approved	10.3 Idhini

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
1.1 Authorization and Powers	These Guidelines are issued under Section 6 (2) (e) and 11 (b) of the Insurance Act Cap 394 which mandate the Authority to formulate and enforce standards in the conduct of the business of insurance which shall be observed by insurance registrants.	1.1 Idhini na Mamlaka	Mwongozo huu umetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2) (e) na 11 (b) cha Sheria ya Bima Sura Na. 394 ambacho kinaiaigiza Mamlaka kuweka vigezo vya uendeshaji wa shughuli za bima ambavyo vitatakiwa kuzingatiwa na watoa huduma za bima.
1.2 Citation	This Guidelines may be cited as “ <i>Guidelines on Corporate Good Governance for Insurers, 2025.</i> ”	1.2 Nukuu	Miongozo hii itajulikana kama “ <i>Miongozo ya Mahitaji ya Utawala Bora kwa Kampuni za Bima Tanzania 2025</i> ”
1.3 Background and Rationale	<p>1.3.1 Insurers are required to have a robust system of governance involving Board of Directors, Management and Control Functions. These systems need to properly guided in order to ensure their relevance and effectiveness.</p> <p>1.3.2 The rationale of corporate governance includes improved corporate performance, capital formation, maximization of shareholders value and protection of policyholders and other stakeholders’ rights.</p>	1.3 Usuli na Mantiki	<p>1.3.1 Utawala wa kampuni ni mfumo wa kanuni, taratibu na michakato inayotumiwa kuongoza na kusimamia kampuni. Unahusu jinsi kampuni zinavyoongozwa pamoja na kubainisha nani ana mamlaka na uwajibikaji, na maamuzi ya kampuni.</p> <p>1.3.2 Umuhimu wa utawala bora katika utendaji wa kampuni, uwepo wa mtaji, uboreshaji wa thamani ya wanahisa na kulinda haki za wakatabima na wadau wengine.</p>

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
	1.3.3 These Guidelines aim to improve insurer's corporate governance, risk management, protect the policyholders interest, maintain integrity of persons dealing with insurance business and improve internal controls necessary to enhance insurers' business performance.		1.3.3 Miongozo hii inalenga kuboresha usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani unaohitajika ili kuimarisha ufanisi wa biashara ya kampuni ya bima.
1.4 Application	1.4.1 These Guidelines shall apply to all insurers and reinsurers (herein referred to as "insurers") registered and licensed by the Authority to carry on insurance business in Tanzania.	1.4 Matumizi	1.4.1 Miongozo hii itatumika na kampuni zote za bima, na bima mtawanyo, (hapa zinajulikana kama "kampuni za bima") zilizosajiliwa na kupewa leseni na Mamlaka kufanya biashara ya bima nchini Tanzania.
1.5 Objectives	<p>1.5.1 To promote and maintain public confidence in the insurance business;</p> <p>1.5.2 To establish effective standards on corporate governance in the insurance market, consistent with the Act, national laws, and good international practices.</p> <p>1.5.3 To streamline the roles of board of directors and senior management of an insurer in overseeing the insurer's business as well as establishing mechanism for holding members of</p>	1.5 Malengo	<p>1.5.1 Kuchangia katika kukuza na kudumisha imani ya biashara ya bima kwa umma.</p> <p>1.5.2 Kuweka viwango madhubuti vya utawala bora kwenye soko la bima kwa kuzingatia Sheria ya Bima na Sheria nyingine muhimu za kitaifa pamoja na Kanuni bora za kimataifa.</p> <p>1.5.3 Kuboresha majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi na Maafisa waandamizi wa kampuni za bima katika kusimamia biashara ya kampuni ya bima pamoja na kuweka utaratibu</p>

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
	<p>the board and management accountable and responsible for their actions,</p> <p>1.5.4 To ensure that insurers are managed in a sound and prudent manner by having in place systems for identifying, assessing, monitoring, and mitigating the risks that affect their ability to meet their obligations to policyholders.</p> <p>1.5.5 To ensure that all key persons in the control functions of an insurer are and remain fit and suitable to fulfil their respective roles.</p>		<p>wa uwajibikaji na uwazi wa wajumbe wa bodi na menejimenti kwa utendaji wao.</p> <p>1.5.4 Kuhakikisha kwamba kampuni za bima zinasimamiwa kwa busara kwa kuwa na mifumo madhubuti ya kutambua, kutathmini, kufuatilia na kupunguza vihatarishi vinavyoathiri uwezo wa kutimiza wajibu wao kwa wabima.</p> <p>1.5.5 Kuhakikisha kuwa wataalam wote wa bima wanaojihusisha na soko la bima wana utaalam wa kutosha na uadilifu katika kutekeleza majukumu yao.</p>
1.6 Interpretation	<p>1.6.1 In these Guidelines, unless the context requires otherwise; reference to the following words shall have the meaning assigned in this Guideline:</p> <p>“Act”- means the Insurance Act Cap 394</p> <p>“Authority”- means Tanzania Insurance Regulatory Authority as established by Section no. 5 (1) of the Insurance Act, Cap 394</p>	1.6 Tafsiri	<p>1.6.1 Katika Miongozo hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo; rejeo la maneno yafuatayo litakuwa na maana iliyotolewa katika Miongozo hii:</p> <p>“Sheria” maana yake ni Sheria ya Bima, Sura ya 394</p> <p>“Mamlaka” - maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kama ilivyoanzishwa na kifungu Na. 5 (1) cha Sheria ya Bima, Sura 394.</p>

SECTION ONE: INTRODUCTION	SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI
<p>“Alternate Director” means a person appointed to temporarily act in place of a substantive Board Director during the latter’s absence, exercising the Director’s powers only for that period, and subject to regulatory approval and fit and proper requirements.</p> <p>“Board” means the Board of Directors of an insurer.</p> <p>“Corporate good governance” means the system of rules, practices and processes by which a company is directed and controlled. It refers to the way in which companies are governed and to what purpose as well as identifying who has power and accountability, and who makes decisions.</p> <p>“Director” - shall have the meaning ascribed to it in Section No. 2 of the Companies Act.</p> <p>“Senior Management”- means a team of individuals at the highest level of the insurer’s management who have the day-to-day responsibilities of managing the insurance</p>	<p>“Mkurugenzi Mbadala” ni mtu anayeteuliwa kwa muda kuchukua nafasi ya mkurugenzi wa bodi pale anapokuwa hayupo au hawezi kutekeleza majukumu yake, na hutekeleza majukumu hayo kwa kipindi hicho tu, kwa kuzingatia idhini ya Mamlaka na vigezo vya kufaa na kustahili.</p> <p>“Bodi” maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni ya bima.</p> <p>“Utawala Bora” maana yake ni mfumo wa kanuni, taratibu, na michakato ambayo kampuni huongozwa, kuendeshwa na kusimamiwa. Ni namna kampuni zinavyotawaliwa, malengo yanayoongoza utawala huo, pamoja na kubainisha nani ana mamlaka, nani mwenye dhamana ya kufanya maamuzi, na nani anawajibika kwa maamuzi hayo.</p> <p>“Mkurugenzi” - itakuwa na maana iliyoainishwa katika Kifungu Na. 2 cha Sheria ya kampuni.</p> <p>“Viongozi Waandamizi”- maana yake ni timu ya watu katika ngazi ya juu ya usimamizi wa kampuni ya bima ambao wana majukumu ya kila siku ya kusimamia biashara ya bima.</p>

SECTION ONE: INTRODUCTION	SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI
<p>business, including but not limited to Chief Executive Officer, Chief Operating Officer, Chief Finance Officer and Heads of Control Functions.</p> <p>“Principal Officer” - means a person responsible for the daily management of the principal office of the insurer, as defined under Section No. 3 of the Act.</p> <p>“Non-Executive Director” - means an individual not involved in the day-to-day management of the insurer and is not a salaried employee of an insurer or its subsidiaries.</p> <p>"Insurance business" - shall have the meaning ascribed to it in Section No. 3 of the Act.</p> <p>"Insurer" - means a person carrying on insurance business other than a broker or agent;</p> <p>“Independent Director”- means to a member of a board of directors who does not have a material</p>	<p>"Afisa Mkuu" - maana yake ni mtu anayehusika na usimamizi wa kila siku wa ofisi kuu ya kampuni ya bima, kama ilivyofafanuliwa chini ya Kifungu Na. 3 cha Sheria ya Bima.</p> <p>“Mkurugenzi Asiyekuwa Mtendaji” - maana yake ni mtu asiyehusika katika usimamizi wa kila siku wa kampuni ya bima na si mfanyakazi anayelipwa mshahara kutoka katika kampuni ya bima au kampuni zake tanzu.</p> <p>"Biashara ya bima" - itakuwa na maana iliyoainishwa katika Kifungu Na. 3 cha Sheria.</p> <p>"Kampuni ya Bima" - maana yake ni mtu anayefanya biashara ya bima isipokuwa dalali au wakala;</p> <p>"Mkurugenzi wa kujitegemea"- maana yake ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ambaye hana</p>

SECTION ONE: INTRODUCTION	SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI
<p>relationship with a company and is neither part of its executive team nor involved in the day-to-day operations of the company.</p> <p>"Actuary" - shall have the meaning ascribed to it in Section No. 3 of the Act;</p> <p>"Independent Actuary"- means an actuary who has not been previously employed by the insurer in any capacity, has no personal relation to the insurer, its affiliates, associates, senior managers or its service providers.</p> <p>"Independent Auditor" - means the auditor appointed under section 36 (1) of the Insurance Act and has not been previously employed by the Insurer in any capacity, has no personal relation to the insurer, its affiliates, associates, its senior managers or its service providers.</p> <p>"Key persons in Control functions"- comprise the head of Actuarial Function, head of the</p>	<p>uhusiano wa nyenzo na kampuni na si sehemu ya timu yake ya utendaji wala kushiriki katika shughuli za kila siku za kampuni.</p> <p>"Mtakwimu bima" - itakuwa na maana iliyoainishwa katika Kifungu Na. 3 cha Sheria;</p> <p>"Mtakwimu Bima Huru" - maana yake ni mtakwimu bima ambaye hajawahi kuajiriwa na kampuni ya bima katika nafasi yoyote na asie na uhusiano wa kibinafsi na kampuni ya bima, washirika wake, wasimamizi waandamizi au watoa huduma wake.</p> <p>"Mkaguzi Huru" - maana yake ni mkaguzi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Bima na hajawahi kuajiriwa hapo awali na kampuni ya Bima kwa nafasi yoyote, hana uhusiano wa kibinafsi na kampuni ya bima, washirika wake, wasimamizi waandamizi au watoa huduma wake.</p> <p>"Watu Muhimu katika Shughuli za Udhibiti" wanajumuisha mkuu wa Shughuli ya</p>

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
	<p>Compliance function, head of Risk Management Function, head of Internal Audit Function, External Auditor and Appointed Actuary.</p> <p>“Significant Owners” means a person who owns ten percent or more of the voting share of the insurer licensed under the Insurance Act.</p> <p>“Specified Officer” means any officer or employee who possesses prerequisite qualifications and is mainly responsible for the soliciting or procuring of insurance business.</p>		<p>Utakwimubima, Mkuu wa Shughuli ya Matekelezo, Mkuu wa Shughuli ya Usimamizi wa Vihatarishi, mkuu wa Ukaguzi wa Ndani, Mkaguzi wa Nje na Mtakwimubima mteule.</p> <p>"Wamiliki Muhimu" maana yake ni mtu ambaye anamiliki asilimia kumi au zaidi ya haki ya kupiga kura katika kampuni ya bima iliyosajiliwa chini ya Sheria ya bima.</p> <p>"Afisa Aliyeainishwa" maana yake ni afisa au mfanyakazi yeyote ambaye ana sifa zinazohitajika na anawajibika zaidi kwa kutafuta au kupata biashara ya bima.</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
2.1 Board Oversight	<p>2.1.1 The Oversight function of each insurer shall be entrusted with the Board. The Board shall be responsible for:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. To review corporate strategies, shape the culture, set the tone at the top, and promote the organization's vision, values, and core beliefs. ii. To oversee senior management's collective ownership and individual accountability for regulatory compliance and risk management. iii. To develop and implement the Board Charter consistent with these Guidelines. iv. To appoint the Senior Management of the Insurer. v. To approve the annual budget, business plan, and strategic plan; and review the insurer's performance. 	2.1 Usimamizi wa Bodi	<p>2.1.1 Kazi ya usimamizi wa kila kampuni ya bima itakabidhiwa kwa Bodi. Bodi itakuwa na jukumu la:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. utekelezaji, matumizi, na ufanisi wa jumla wa mfumo wa utawala kwa kuzingatia asili, kiasi, na hatari za shughuli, kuhakikisha usimamizi wa busara na uwazi. ii. usimamizi mzuri na muundo, uwajibikaji kwa utendaji na mwenendo wa kampuni ya bima, ambayo ni muhimu kwa utawala bora. iii. Kutoa mwongozo wa kimkakati, mwelekeo wa sera, na uwajibikaji kwa wanahisa, wabima, na wadau iv. Kuteua afisa mwandamizi wa kampuni ya bima v. Kupitisha bajeti, mpango wa biashara na mpango mkakati, na kufanya mapitio ya utendaji wa kampuni ya bima

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	<ul style="list-style-type: none"> vi. To establish policies and monitor operations to ensure the insurer complies with governing laws and regulations. vii. To plan for capital needs and ensure the insurer is adequately capitalized at all times. viii. To establish standards of business conduct and ethical behavior for directors, senior management, and key persons in control functions. ix. To establish Board Committees with specific responsibilities which shall be incorporated into the Board Charter. x. To receive, analyze, and implement internal and external Auditors' recommendations. 		<ul style="list-style-type: none"> vi. Kutunga sera na kusimamia utekelezaji ili kuhakikisha kampuni ya bima inafanya biashara kwa kuzingatia sheria zilizopo vii. Kupanga mahitaji ya mtaji ili kuhakikisha kampuni ya bima inakuwa na mtaji toshelevu muda wote wa ufanyaji biashara viii. Kuweka viwango katika ufanyaji biashara na maadili kwa viongozi waandamizi wa kampuni ya bima katika maeneo yote muhimu ya kampuni ix. Kuweka Kamati za Bodi na kuzipangia majukumu mahususi ambayo yataainishwa katika mwongozo wa utendaji wa shughuli za Bodi x. Kupokea, kuchambua na kutekeleza ushauri au mapendekezo ya wakaguzi wa ndani na nje

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	<ul style="list-style-type: none"> xi. To be accountable for all aspects of governance, including but not limited to decision-making. xii. To define and clarify responsibilities for operational, control, and reporting processes through organizational structures. xiii. To ensure organizational design is understood by managers, employees, and external stakeholders. 		<ul style="list-style-type: none"> xi. Kuwajibika katika masuala yote ya utawala bora ikiwemo kutoa maamuzi xii. Kutafsiri na kufafanua majukumu ya kiuendeshaaji na taratibu za kutoa taarifa kwa kuzingatia muundo wa kampuni xiii. Kuhakikisha muundo wa kampuni unafahamika na mameneja, wafanyakazi na wadau wa nje
2.2 Board Requirements	<p>2.2.1 Insurers shall ensure that at least one-third (1/3) of their Board members are Independent Directors, in line with Section 27(1) of the Act, and shall include at least one member of the opposite gender to promote diversity.</p> <p>2.2.2 The tenure limit shall apply only to Independent Non-Executive Directors, with a maximum cumulative tenure of fifteen (15) years renewable twice.</p>	2.2 Mahitaji ya Bodi	<p>2.2.1 Kampuni za bima zitahakikisha kuwa angalau theluthi moja (1/3) ya wajumbe wa Bodi yao ni Wakurugenzi Huru, kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1) cha Sheria, na kwamba Bodi inajumuisha angalau mjumbe mmoja wa jinsia tofauti ili kukuza uwiano na utofauti wa kijinsia.</p> <p>2.2.2 Kikomo cha muda wa kuhudumu kitatumika kwa Wakurugenzi Wasio</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	<p>Other Non-Executive Directors may serve beyond this period on a comply-or-explain basis, while shareholder-nominated directors exceeding the prescribed ownership threshold are exempt from the tenure cap but remain subject to fit and proper requirements and periodic re-election.</p> <p>2.2.3 An Independent Non-Executive Director who, as at the date these Guidelines come into effect, has served for a cumulative period of fifteen (15) years or more shall be allowed a moratorium period of up to three (3) years or until the expiry of the current term of office, whichever occurs first, after which the Director shall cease to serve in that capacity.</p>		<p>Watendaji Huru pekee, kwa muda wa juu wa miaka kumi na tano (15), kinachoweza kuhuishwa hadi mara mbili. Wakurugenzi wengine Wasio Watendaji wanaweza kuendelea kuhudumu zaidi ya hapo, huku Wakurugenzi waliopendekezwa na wanahisa wenye umiliki mkubwa hawatawekewa kikomo cha muda, lakini wataendelea kuzingatia vigezo vya kufaa na kustahili pamoja na taratibu za kuchaguliwa upya.</p> <p>2.2.3 Mkurugenzi Huru Asiye Mtendaji ambaye, kufikia tarehe ya kuanza kutumika kwa Miongozo hii, amehudumu kwa jumla ya miaka kumi na tano (15) au zaidi, ataruhusiwa kuendelea kuhudumu kwa kipindi cha mpito kisichozidi miaka mitatu (3) au hadi kumalizika kwa muhula wake wa sasa, chochote</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	<p>2.2.4 The Board shall ensure there is a clear separation between management and Board functions.</p> <p>2.2.5 Any appointment of alternate directors must receive approval from the Authority and comply with Section 27 of the Act.</p> <p>2.2.6 An Alternate Director temporarily replaces a substantive director to maintain Board continuity and quorum and to exercise delegated duties for that period only.</p>		<p>kitakachotokea kwanza, kabla ya kuacha rasmi nafasi hiyo.</p> <p>2.2.4 Bodi itahakikisha kuna mgawanyo wazi kati ya majukumu ya uendeshaji wa kampuni na Bodi.</p> <p>2.2.5 Uteuzi wowote wa wakurugenzi mbadala lazima upate idhini kutoka kwa Mamlaka na uzingatie Kifungu cha 27 cha Sheria.</p> <p>2.2.6 Mkurugenzi Mbadala huchukua nafasi ya mkurugenzi halisi kwa muda mfupi ili kuhakikisha mwendelezo wa kazi za Bodi na kutimia kwa akidi, na hutekeleza majukumu aliyokabidhiwa kwa kipindi hicho tu.</p>
2.3 Independent Directors	<p>2.3.1 Subject to 2.2.1 an independent director shall meet the following criteria –</p> <p>i. Recruited in a transparent and competitive manner;</p>	2.3 Wakurugenzi Huru	<p>2.3.1 Kwa kuzingatia 2.2.1 mkurugenzi huru anatakiwa kuwa na vigezo vifuatavyo –</p> <p>i. Aliyepatikana kwa njia ya uwazi na yenye ushindani.</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	<p>ii. Not had any business relationship with the Insurer (other than service as a director);</p> <p>iii. Is not, in the opinion of the Commissioner unfit to hold such position on grounds of lacking independence or having a vested interest in the insurer or any other public and market interest.</p>		<p>ii. Asiwe na uhusiano wowote wa kibiashara na kampuni ya bima (zaidi ya huduma kama mkurugenzi).</p> <p>iii. Kwa maoni ya Kamishna, hana sifa zisizomruhusu kushika nafasi hiyo kutokana na kukosa uhuru au kuwa na maslahi binafsi katika kampuni ya bima husika au katika maslahi ya umma na soko kwa ujumla.</p>
2.4 Structure and Qualifications of the Board	<p>2.4.1 A Board shall be composed of a minimum of five (5) member.</p> <p>2.4.2 Board members shall have the necessary skills, knowledge, and experience to direct and oversee the insurer in a professional manner.</p> <p>2.4.3 Without prejudice to the generality of item 2.4.2, the board shall ensure that the majority of its members possess requisite expertise and skills commensurate to nature, scale and complexity of insurer's business, as stipulated in the Appendix 1.</p>	2.4 Muundo wa Bodi	<p>2.4.1 Bodi itaundwa na wajumbe wasiopungua watano (5).</p> <p>2.4.2 Wajumbe wa Bodi wanatakiwa kuwa na ujuzi, maarifa, na uzoefu unaohitajika ili kuelekeza na kusimamia kampuni ya bima kwa kuzingatia utaalum.</p> <p>2.4.3 Bila kuathiri masharti ya jumla yaliyotajwa katika kipengele cha 2.4.2, Bodi itahakikisha kuwa wajumbe wake wengi wanamiliki utaalumu na ujuzi unaolingana na aina, ukubwa, na utata wa shughuli za kampuni ya bima, kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho Na. 1.</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	2.4.4 Every Board member shall meet fit-and-proper requirements as prescribed by the Authority.		2.4.4 Kila mjumbe wa Bodi anapaswa kukidhi sifa na mahitaji yanayotakiwa kama inavyoelekezwa na Mamlaka.
2.5 Chairperson of the Board	<p>2.5.1 The Chairperson of the Board shall be a non-executive and independent director.</p> <p>2.5.2 The principal responsibilities of the Chairperson shall include ensuring adherence to the responsibilities outlined in section 2.1</p>	2.5 Mwenyekiti wa Bodi	<p>2.5.1 Mwenyekiti wa Bodi anatakiwa kuwa mkurugenzi huru na asiye mtendaji katika kampuni.</p> <p>2.5.2 Majukumu makuu ya Mwenyekiti yatakuwa pamoja na kuhakikisha uzingatiaji wa majukumu yaliyoainishwa katika kifungu cha 2.1</p>
2.6 Establishment of Board Committees	<p>2.6.1 Subject to Section 42 and 49(1) of the Act, the Board shall establish Board committees to assist in discharging its responsibilities related to audit and investment matters respectively.</p> <p>2.6.2 Without prejudice to item 2.7.1, the Board may form any additional committees deemed necessary for effective discharge of its functions. Provided that the following functions</p>	2.6 Uundwaji wa Kamati za Bodi	<p>2.6.1 Kwa mujibu wa Sehemu ya 42 na 49(1) ya Sheria, Bodi itaanzisha kamati za Bodi kusaidia katika kutekeleza majukumu yake yanayohusiana na masuala ya ukaguzi na uwekezaji.</p> <p>2.6.2 Bila kuathiri kipengele cha 2.7.1 Bodi itakuwa na uhuru wa kuunda idadi yoyote ya kamati inazoon kuwa ni muhimu kwa utawala bora. Hata hivyo, ni muhimu kuhakikisha</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	<p>must be discharged through the committees</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Underwriting and Claims Management; ii. Risk and Compliance; iii. Information and Communication Technology; iv. Policyholders and Beneficiaries Protection; v. Ethics and Professional conduct; and vi. Human resources <p>2.6.3 The Board shall specify and document terms of reference for each of its committees in the manner and format described by the Authority as stipulated in Appendix 2.</p>		<p>kwamba kazi zifuatazo zimezingatiwa kupitia kamati hizi:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Mkakati wa Uandikishaji na Usimamizi wa Madai; ii. Vihatarishi na Ufuataji; iii. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; iv. Ulinzi wa haki za wakataka na wanufaika wa bima; v. Maadili na Mwenendo wa Kitaaluma; na vi. Rasilimali watu. <p>2.6.3 Bodi itabainisha na kuweka kumbukumbu za hadidu za rejea kwa kila moja ya kamati zake kwa namna na muundo unaoelekezwa na Mamlaka, kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho Na. 2.</p>
2.7 Board Audit Committee	<p>2.7.1 An insurer's board audit committee shall be constituted in accordance with Section 42 of the Act.</p>	2.7 Kamati ya Ukaguzi ya Bodi	<p>2.7.1 Kamati ya ukaguzi ya Bodi ya kampuni ya bima itaundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 42 cha Sheria ya bima.</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	<p>2.7.2 Subject to Regulation 40 of the insurance Regulations of 2009, the audit committee shall functions as stipulated in Appendix 3</p> <p>2.7.3 The Authority may specify any additional responsibilities to be discharged by the insurer's audit committee as and when deemed appropriate.</p>		<p>2.7.2 Kwa kuzingatia Kanuni ya 40 ya Bima ya mwaka 2009, kamati ya ukaguzi itatekeleza majukumu kama ilivyoinishwa katika Kiambatisho Na. 3.</p> <p>2.7.3 Mamlaka inaweza kubainisha majukumu yoyote ya ziada yatakayotekelezwa na kamati ya ukaguzi ya Bodi inapoonekana inafaa.</p>
2.8 Board Investment Committee	<p>2.8.1 An insurer's board investment committee shall be constituted in accordance with Section 49(1) of the Act.</p> <p>2.8.2 Subject to Section 49 (2) (a) and (b) of the Act, the investment committee shall perform functions as prescribed in Appendix 3</p> <p>2.8.3 The Authority may specify any additional responsibilities to be discharged by the insurer's investment committee as and when deemed appropriate.</p>	2.8 Kamati ya Bodi ya Uwekezaji	<p>2.8.1 Kamati ya Uwekezaji ya Bodi ya kampuni ya bima itaundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 49(1) cha Sheria ya Bima.</p> <p>2.8.2 Kwa kuzingatia Kifungu cha 49 (2) (a) na (b) cha Sheria ya Bima, Kamati ya uwekezaji ya Bodi itatekeleza majukumu kama ilivyianishwa katika Kiambatisho Na. 3</p> <p>2.8.3 Mamlaka inaweza kubainisha majukumu yoyote ya ziada yatakayotekelezwa na kamati ya uwekezaji ya bima pale itakapoona inafaa.</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
2.9 Other Board Committee	<p>2.9.1 The Board is required to report the establishment of any additional committees to the Authority, including the terms of reference for each committee.</p> <p>2.9.2 Without prejudice to item 2.8.2, other committee formulated by the Board shall perform functions as prescribed in Appendix 3.</p>	2.9 Kamati nyingine za Bodi	<p>2.9.1 Bodi inatakiwa kutoa taarifa kwa Mamlaka kuhusu kuanzishwa kwa kamati yoyote ya ziada, ikijumuisha masharti ya marejeo kwa kila kamati.</p> <p>2.9.2 Bila kuathiri kipengele cha 2.8.2, Kamati nyingine zinazoundwa na Bodi zitatekeleza majukumu kama yanavyoainishwa katika Kiambatisho Na. 3.</p>
2.10 Senior Management and Chief Executive Officer and Principal Officer	<p>2.10.1 The Chief Executive Officer shall be responsible for the strategic leadership and operational management of the insurer.</p> <p>2.10.2 The Principal Officer shall be the primary liaison with the Authority and shall be responsible for ensuring the insurer's compliance with statutory, regulatory, and legal obligations.</p>	2.10 Viongozi Waandamizi na Mtendaji Mkuu na Afisa Mkuu	<p>2.10.1 Mtendaji Mkuu atawajibika kwa uongozi wa kimkakati na usimamizi wa uendeshaji wa shughuli za kila siku za kampuni ya bima.</p> <p>2.10.2 Afisa Mkuu atakuwa kiungo kikuu kati ya kampuni ya bima na Mamlaka, na atawajibika kuhakikisha kuwa kampuni inazingatia matakwa yote ya kisheria, kanuni na masharti ya udhibiti.</p>

SECTION TWO: GOVERNANCE OVERSIGHT AND STRUCTURE		SEHEMU YA PILI: USIMAMIZI NA MUUNDO WA UANGALIZI WA UTAWALA	
	2.10.3 The responsibilities of senior management will be as outlined in Appendix 4.		2.10.3 Majukumu ya viongozi waandamizi yatazingatia yaliyoainishwa katika Kiambatisho Na. 4.

SECTION THREE: CAPACITY BUILDING FOR BOARD AND MANAGEMENT			SEHEMU YA TATU: KUJENGA UWEZO KWA BODI, WASIMAMIZI WAANDAMIZI NA WAFANYAKAZI				
3.1	Capacity Building for Board and Management	3.1.1	Cognizant of the dynamic nature of corporate governance, industry practices, and regulatory requirements, the Board shall establish and implement a robust continuous education and professional development program for its members, management and staff.	3.1	Kujenga Uwezo kwa Bodi na Menejimenti	3.1.1	Kwa kutambua mabadiliko katika utawala bora, uzoefu katika utendaji na mahitaji ya usimamizi, Bodi itaweka utaratibu thabiti wa kujenga uwezo wa kielimu kwa wajumbe wa Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa kampuni ya bima.
		3.1.2	Each member of the Board and Management shall attend at least two relevant industry seminars, conferences, and forums per year to gain insights into industry developments, emerging technologies, and market trends.			3.1.2	Kila mjumbe wa Bodi na Menejimenti anatakiwa kuhudhuria mafunzo angalau mara mbili kupitia semina na mikutano kila mwaka ili kupata uelewa wa maendeleo ya soko, teknolojia mpya na mwenendo wa masoko
		3.1.3	The continuous education and professional development program for Board and Management referred to under item 3.1.1 shall be those provided by a reputable institution duly authorized by TCU, NACTVET or other relevant authorities as stipulated in Appendix 5.			3.1.3	Elimu endelevu na programu ya maendeleo ya tasnia kwa Bodi na Menejimenti itakuwa na zile zilizoadhinishwa na taasisi zinazotambuliwa na TCU, NACTVET au taasisi nyingine kama ilivyoanishwa katika Kiambatisho Na.5.

SECTION THREE: CAPACITY BUILDING FOR BOARD AND MANAGEMENT		SEHEMU YA TATU: KUJENGA UWEZO KWA BODI, WASIMAMIZI WAANDAMIZI NA WAFANYAKAZI	
	<p>3.1.4 The company shall provide directors with educational resources such as research reports, articles, and online courses to enhance their understanding of key topics related to corporate governance and market dynamics.</p> <p>3.1.5 The Board shall foster a culture of continuous learning and knowledge sharing among directors, encouraging collaborative discussions and the exchange of experiences to enrich collective wisdom and decision making capacity.</p>		<p>3.1.4 Kampuni itatoa kwa wakurugenzi rasilimali za elimu, kama vile ripoti za utafiti, makala, na kozi za mtandaoni, ili kuimarisha uelewa wao wa mada muhimu zinazohusiana na utawala wa ushirika na mienendo ya soko.</p> <p>3.1.5 Bodi itakuza utamaduni wa kujifunza na kubadilishana maarifa miongoni mwa wakurugenzi, kuhamasisha majadiliano ya ushirikiano na kubadilishana uzoefu ili kuongeza hekima ya pamoja na uwezo wa kufanya maamuzi.</p>

SECTION FOUR: SUCCESSION PLANNING		SEHEMU YA NNE: MPANGO WA URITHISHANAJI MADARAKA	
4.1 Succession Planning Process	4.1.1 The insurer shall establish and maintain a documented contingency and capacity development plan for the Board, Senior Management, and key control functions. The plan shall ensure preparedness for unexpected leadership changes, support internal skills development and competence and promote flexibility and merit-based advancement, without requiring the premature designation of specific successors.	4.1 Mchakato wa Urithishanaji Madaraka	4.1.1 Kampuni ya bima itaunda na kudumisha mpango uliandikwa wa dharura na uendelezaji wa uwezo kwa ajili ya Bodi, Menejimenti na majukumu muhimu ya udhibiti. Mpango huo utahakikisha utayari wa kampuni kukabiliana na mabadiliko ya ghafla ya uongozi, maendeleo ya ujuzi na uwezo wa ndani na kukuza kuboreshwa kwa watendaji kwa kuzingatia sifa na uwezo, bila kuhitaji uteuzi wa mapema wa warithi wa nafasi husika.
	4.1.2 The insurer shall, at least annually and whenever there is a material change in the organisational structure or key positions, monitor and review the effectiveness of the succession, contingency and capacity development plan, including the adequacy of internal capacity and readiness to respond to unexpected changes in leadership.		4.1.2 Kampuni ya bima angalau mara moja kwa mwaka na kila mara kunapokuwa na mabadiliko makubwa katika muundo wa kampuni au katika nafasi muhimu, atafuatilia na kufanya mapitio ya ufanisi wa mpango wa urithi wa uongozi, mpango wa dharura na ujengeaji uwezo, ikijumuisha tathmini ya uwiano na kukidhi uwezo wa ndani na utayari wa

SECTION FOUR: SUCCESSION PLANNING		SEHEMU YA NNE: MPANGO WA URITHISHANAJI MADARAKA	
	<p>4.1.3 The succession, contingency and capacity development plan referred to under 4.1.1 shall be prepared in accordance with Appendix 6 and shall be submitted to the Authority on an annual basis, together with a report on its implementation and any material changes made during the year.</p> <p>4.1.4 Each insurer shall adhere to and implement the succession, contingency and capacity development plan submitted to and approved by the Authority</p>		<p>kukabiliana na mabadiliko yasiyotegemewa katika uongozi.</p> <p>4.1.3 Mpango wa urithi wa uongozi, mpango wa dharura na ujengeaji uwezo unaorejewa katika kifungu cha 4.1.1 utaandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Kiambatisho Na. 6 na kuwasilishwa kwa Mamlaka kila mwaka, ukiambatanisha taarifa ya utekelezaji wa mpango huo na mabadiliko yote muhimu yaliyofanyika katika kipindi husika.</p> <p>4.1.4 Kila kampuni ya bima itazingatia na kutekeleza mpango wa urithi wa uongozi, mpango wa dharura na ujengeaji uwezo uliowasilishwa kwa, na kuidhinishwa na, Mamlaka.</p>

SECTION FIVE: PERFORMANCE EVALUATION		SEHEMU YA TANO: TATHMINI YA UTENDAJI	
5.1 Board Evaluation	<p>5.1.1 The Board shall appoint an external auditor approved by the Authority to assess the effectiveness of the Board and its Committees, in accordance with the criteria set out in Appendix 7.</p> <p>5.1.2 The Board shall provide an appraisal to the Commissioner on results of its evaluation annually, within a period of 90 days of end of the financial year of the insurer, in format prescribed in Appendix 7.</p>	5.1 Tathmini ya Utendaji wa Bodi	<p>5.1.1 Bodi itateua mkaguzi wa nje aliyeidhinishwa na Mamlaka kufanya tathmini ya ufanisi wa Bodi na Kamati zake, kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika Kiambatisho cha 7.</p> <p>5.1.2 Bodi itakutana katika kikao cha tathmini ya utendaji wake ili kujadili tathmini ya utendaji wa majukumu yake na kuwasilisha taarifa kwa Kamishna kila mwaka kama ilivyoanishwa katika Kiambatisho Na 7.</p>
5.2 Evaluation of Board Committees	<p>5.2.1 Each committee of the Board shall annually conduct a self-evaluation and report the results to the Board.</p> <p>5.2.2 The evaluation process must compare the performance of the committee with the requirements of its Terms of Reference.</p>	5.2 Tathmini ya Kamati za Bodi	<p>5.2.1 Kila kamati ya Bodi itafanya tathmini binafsi na kuripoti matokeo kwa Bodi kila mwaka.</p> <p>5.2.2 Mchakato wa tathmini utalinganisha utendaji kazi wa kamati na matakwa ya Hadidu zake za Rejea.</p>
5.3 Evaluation of Chief Executive Officer or Principal Officer	<p>5.3.1 The Board shall establish policies and procedures for the evaluation of the Principal Officer.</p> <p>5.3.2 The evaluation shall be based on set criteria including among other things compliance with the Act, Regulations, Guidelines and</p>	5.3 Tathmini ya Afisa Mtendaji Mkuu au Afisa Mkuu	<p>5.3.1 Bodi itaweka sera na taratibu za kufanya tathmini ya utendaji kwa Afisa Mkuu.</p> <p>5.3.2 Tathmini ya utendaji wa Afisa mtendaji au watendaji waandamizi itazingatia pamoja na mambo mengine utekelezaji wa matakwa ya</p>

SECTION FIVE: PERFORMANCE EVALUATION	SEHEMU YA TANO: TATHMINI YA UTENDAJI
<p>procedures set by the Authority, succession plan, capacity building, complaint handling, performance of the insurer's business, the accomplishment of long-term strategic objectives and performance of senior management.</p> <p>5.3.3 The evaluation shall be conducted annually under the oversight of the Board and report shall be submitted to the Authority;</p> <p>5.3.4 The Authority through its Key Performance Indicators for assessing performance of company's senior management officers may grant or reject No Objection for applicants for vacant position.</p>	<p>Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa na Mamlaka, utekelezaji wa mpango wa urishishaji uongozi wa kampuni, kujenga uwezo kwa wafanyakazi, utatuzi wa malalamiko na utekelezaji wa malengo ya kimkakati ya kampuni ya bima</p> <p>5.3.3 Tathmini ya utendaji itafanyika kila mwaka chini ya uangalizi wa Bodi na taarifa ya matokeo ya tathmini kuwasilishwa kwa Mamlaka.</p> <p>5.3.4 Mamlaka kwa kuzingatia vigezo vya utendaji kwa watendaji waandamizi wa kampuni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na inaweza kuridhia au kutoridhia kutoa kibali kwa muhusika kushika au kuendelea kushika nafasi husika</p>

SECTION SIX: INTERNAL GOVERNANCE MECHANISMS		SEHEMU YA SITA: MIKAKATI YA NDANI YA UTAWALA	
6.1 Internal Good Governance Mechanism	6.1.1 The Authority mandates insurers to establish and maintain an effective system of internal controls.	6.1 Mkakati wa Ndani wa utawala bora	6.1.1 Mamlaka inataka kampuni za bima kuanzisha na kudumisha mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani.
	6.1.2 The internal control system must ensure effective operations, risk control, prudent business conduct, reliable reporting, and compliance with laws, regulations, and internal policies.		6.1.2 Mfumo wa udhibiti wa ndani lazima uhakikishe uendeshaji mzuri, udhibiti wa hatari, mwenendo wa busara wa biashara, utoaji wa taarifa za kuaminika, na ufuataji wa sheria, kanuni, na sera za ndani.
	6.1.3 The internal control system must own, manage, and report on risks, and be accountable for maintaining internal control policies and procedures.		6.1.3 Mfumo wa udhibiti wa ndani lazima uhusishe vitengo vyote na shughuli za kampuni ya bima, uingizwe katika shughuli za kila siku, na ufanyiwe tathmini na kuboreshwa mara kwa mara.
	6.1.4 The insurer shall establish control functions that must include: <ul style="list-style-type: none"> i. Risk management ii. Actuarial iii. Compliance iv. Internal audit 		6.1.4 Kila kampuni ya bima lazima iwe na kazi muhimu zifuatazo: <ul style="list-style-type: none"> i) Usimamizi Vihatarishi ii) Takwimu bima iii) Matekelezo iv) Ukaguzi wa Ndani

	<p>6.1.5 The control functions shall be headed by persons at the managerial level with relevant qualifications and experience.</p> <p>6.1.6 Without prejudice to item 6.2.5, control functions shall adhere to the suitability criteria and perform their functions as prescribed in Appendix 8.</p>		<p>6.1.5 Majukumu muhimu ya kampuni yataongozwa na watu waliopo katika ngazya menejimenti wenye sifa ya kitaaluma na uzoefu</p> <p>6.1.6 Bila kuathiri kipengele cha 6.2.5, vitengo muhimu vitazingatia vigezo stahiki na kutekeleza majukumu yao kama yanavyoainishwa katika Kiambatisho Na. 8.</p>
6.2 Changes to the Risk Management Framework	<p>6.2.1 The Board and Senior Management shall be attentive to Material changes and reasons for the changes to an insurer's risk management framework shall be documented and approved by the Board.</p> <p>6.2.2 Documentation of changes shall be available for internal audit, external audit and the Authority for their respective assessments of the risk management framework.</p>	6.2 Mabadiliko katika Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi	<p>6.2.1 Bodi na Watendaji waandamizi wanapaswa kuzingatia mabadiliko yoyote na sababu za mabadiliko katika mfumo wa usimamizi wa vihatarishi wa kampuni ya bima na kuweka kumbukumbu za kimaandishi na kuidhinishwa na Bodi</p> <p>6.2.2 Taarifa za maandishi kuhusu mabadiliko yaliyofanyika yanapaswa kutolewa kwa mkaguzi wa ndani, mkaguzi wa nje na Mamlaka kwa ajili ya tathmini ya mfumo wa usimamizi wa vihatarishi.</p>

SECTION SEVEN: OUTSOURCING ARRANGEMENTS		SEHEMU YA SABA: MIPANGO YA KUTUMIA HUDUMA ZA NJE	
7.1 Outsourcing agreement	7.1.1 The Board shall be responsible for overseeing the establishment of the control function for the company. In a situation where the Board deems it necessary to perform any outsourcing, they will be required to comply with the Outsourcing Policy approved by the Authority.	7.1 Mahitaji ya Kutumia Huduma za Nje	7.1.1 Bodi itakuwa na jukumu la kusimamia uanzishaji wa jukumu la udhibiti kwa kampuni. Katika hali ambapo Bodi itaona kuna umuhimu wa kupata huduma kutoka nje ya kampuni, , itapaswa kufuata matakwa ya Sera ya Huduma kutoka nje iliyoidhinishwa na Mamlaka.
	7.1.2 An insurer shall assess the need for an outsourcing arrangement or its continued existence depending on materiality of the services to the core of its operations.		7.1.2 Kampuni ya bima itatathmini hitaji la makubaliano ya kutumia huduma za nje au kuendelea kwa uwepo wake kulingana na umuhimu wa huduma hizo kwa msingi wa shughuli zake.
	7.1.3 All insurers intending to outsource any activity or service shall develop an outsourcing policy that at minimum provisions in Appendix 9.		7.1.3 Kampuni za bima zinazokusudia kutumia huduma za nje katika shughuli au huduma yoyote itatakiwa kuandaa sera ya utumiaji wa huduma za nje ambayo itazingatia mahitaji kama yalivyotajwa katika Kiambatisho Na. 9.
	7.1.4 An insurer shall submit the outsourcing policy to the Authority for review and approval before its implementation.		7.1.4 Taasisi inayofanya kazi ya nje lazima iwasilishe sera ya kutumia huduma za

SECTION SEVEN: OUTSOURCING ARRANGEMENTS		SEHEMU YA SABA: MIPANGO YA KUTUMIA HUDUMA ZA NJE	
	<p>7.1.5 Insurers shall take necessary measures to maintain control over outsourced activities to protect policyholders' interests, governance, solvency, and revenue flows, safeguard the integrity and confidentiality of customer data and information in line with applicable laws.</p>		<p>nje kwa Mamlaka kwa mapitio na kupata idhini kabla ya kutekeleza.</p> <p>7.1.5 Kampuni za bima zitachukua hatua zinazohitajika kudumisha udhibiti kuhusu shughuli zilizopelekwa nje ili kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za bima, utawala, uwezo wa kifedha, na mapato. Kutopeana shughuli nje hakutapunguza au kudhoofisha uwezo wa kampuni kufuata majukumu yake ya udhibiti/usahihi wala kuathiri majukumu ya usimamizi ya Mamlaka..</p>
7.2 Scope of Areas for Outsourcing	<p>7.2.1 An insurer shall not seek to outsource the following strategic functions:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. financial management and accounting; ii. compliance function; iii. risk management function; iv. complaints handling; v. underwriting (including reinsurance); vi. Claims management, vii. Administration and Human resource 	7.2 Mipaka ya Maeneo ya Kutumia Huduma za Nje	<p>7.2.1 Kampuni ya bima haipaswi kutafuta na kutumia huduma za nje katika shughuli kuu zifuatazo:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Usimamizi wa kifedha na uhasibu; ii. Majukumu ya matekelezo; iii. Majukumu ya usimamizi wa vihatarishi; iv. kushughulikia malalamiko; v. Kazi za uandikishaji bima (ikiwemo bima mtawanyo)

SECTION SEVEN: OUTSOURCING ARRANGEMENTS	SEHEMU YA SABA: MIPANGO YA KUTUMIA HUDUMA ZA NJE
<p>viii. appointment of agents, surveyors and loss assessors/ adjustors, and</p> <p>ix. any other as specified by the Authority from time to time</p> <p>7.2.2 An insurer shall not outsource its internal audit function to the external auditor or any firm within the auditor's network. Group Internal Audit functions may be used, provided they are independent, report to the Audit Committee, and comply with international internal auditing standards.</p> <p>7.2.3 Where an insurer outsources investment management and fund management, it shall be required to comply with the Outsourcing Policy and Investment Policy approved by the Authority.</p> <p>7.2.4 Each insurer will be required to appoint an independent Insurance Actuary to provide Company Actuary Services in line with the</p>	<p>vi. Ushughulikiaji madai;</p> <p>vii. Shughuli za Utawala na Rasilimali watu</p> <p>viii. Uteuzi wa mawakala, watathmini na wakadiriaji hasara, na</p> <p>ix. Na zingine, kama itakavyoainishwa na Mamlaka.</p> <p>7.2.2 Kampuni ya bima hairuhusiwi kupeleka ukaguzi wa ndani kwa mkaguzi wa nje au kampuni yoyote iliyo ndani ya mtandao wake. Hata hivyo, kitengo cha ukaguzi wa ndani cha kundi kinaweza kutumika endapo ni huru, kinawajibika kwa Kamati ya Ukaguzi, na kinafuata viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ndani.</p> <p>7.2.3 Kampuni za bima zinaweza kutumia huduma za nje kwenye uwekezaji kwa kuzingatia sera ya Huduma za Njen na Sera ya Uwekezaji kama zilivyoidhinishwa na Mamlaka.</p> <p>7.2.4 Kila mtoa bima atatakiwa kutafuta Mthaminishaji Bima wa kujitegemea kwa kufanya kazi za uthaminishaji bima za kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Muongozo kwa</p>

SECTION SEVEN: OUTSOURCING ARRANGEMENTS		SEHEMU YA SABA: MIPANGO YA KUTUMIA HUDUMA ZA NJE	
	requirements of the Guideline to the Insurance Industry on Actuarial Function.		watoa bima kuhusiana na kazi za kuthaminisha bima.

SECTION EIGHT: SUITABILITY OF KEY PERSONS		SEHEMU YA NANE: SIFA ZA WATU MUHIMU	
8.1 Chief Executive Officer or Principal Officer	8.1.1 Chief Executive Officer or Principal Officer shall possess necessary qualifications as prescribed in Regulation 8 of the Insurance Regulations, 2009	8.1 Mtendaji Mkuu au Afisa Mkuu	8.1.1 Afisa Mtendaji Mkuu au Afisa Mkuu anatakiwa kuwa na sifa zinazohitajika kama zilivyoainishwa katika Kanuni ya 8 ya Kanuni za Bima, 2009.
